For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

# KISWAHILI KARATASI YA

1 **UFAHAMU:** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Nchi nyingi duniani zimetia sahihi mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki hizi ni pamoja na uhai, lishe bora inayotosha na makazi bora yaliyo salama. Hali kadhalika, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu inastahili kutolewa bure, iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Isitoshe, mtoto hastahili kupigwa, kudunishwa, wala kubaguliwa kwa namna yoyote ile; iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vinginevyo. Mtoto hapaswi kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kushurutishwa. Vile vile, mtoto ana haki ya kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Fauka ya haya, mtoto anastahili kushirikishwa katika kufanya maamuzi yanayoweza kumwathiri maishani. Pia, mtoto ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum na habari kuhusu masuala mbalimbali. Pamoja na hayo, mtoto anastahili kupendwa na kuheshimiwa kimawazo na kihisia.

Haki za watoto zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, serikali na wazazi wakiwa katika mstari wa mbele. Hii ndiyo sababu serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba na sheria za nchi husika. Yeyote anayezikiuka anapasa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Walakini, haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Kuna watoto ambao hawajawahi hata kupata kibanda cha kuweka ubavu. Wengi wa hawa wamejipata wakiselelea kwenye mitaa na hata majaa ya miji na vijiji ambako hulazimika kupitisha usiku hata katika majira ya kipupwe na masika! Wengine hawapati chakula; licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi; kwani hata awamu moja ni adimu kupata! La kusikitisha ni kwamba wale wanaotarajiwa kuwa **vigogo** wa kuzilinda haki hizi ndio wanaoongoza katika kupalilia ukiukaji wazo. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kushinikizwa kufanya kazi za sulubu kipunda, kunyanyaswa kijinsia, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Baadhi ya wanaohusika na vitendo hivi hasi huwa wazazi au jamaa wa karibu kama vile wajomba, shangazi au wahudumu wa nyumbani.

Madhila yanayowapata watoto hayatokei tu katika mazingira ya nyumbani. Mateso huvuka mipaka na kufikia ngazi ya kimataifa. Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Linalokata maini ni kwamba baadhi ya viongozi katika mataifa haya hawafanyi lolote kuwanusuru. Lao huwa kuwatazama watoto wanaotakiwa kuwalinda wakigeuzwa kuwa mababe wa kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia hulazimika kuvaa mabuti ya kijeshi ambayo **huwa nanga kwao** kubeba, licha ya bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani.

**PILI**

Mojawapo ya mambo ambayo viongozi nchini humu walilenga shabaha kuyafikia baada ya kujinyakulia uhuru ni elimu kwa wote. Hata hivyo, hii imekuwa kama ndoto isiyotabirika katika baadhi ya janibu. Ni kweli kwamba sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi nchini humu inaendelea kutekelezwa. Hata hivyo, asilimia ya watoto na hata watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ingali kubwa. Jukwaa la vijiji nchini humu na hata katika mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu limesheheni idadi kubwa ya watoto wasioenda shuleni. Kichocheo kikuu cha hali hii ni kwamba wazazi na walezi wamejipata katika lindi la ufukara uliokithiri. Hata wanapojitahidi kujinyanyua na **kujikuna wajipatapo** kuyakidhi mahitaji ya kielimu ya wanao, wao hujipata wakitapatapa katika kinamasi hicho hicho cha ulitima. Matokeo ni kwamba watoto wa matajiri wanaendelea kuelimika huku wa maskini wakibakia kwenye kiza cha ujinga. **Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana**.

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima tuungane mikono na kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu utekelezaji wa haki za watoto. Twapaswa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati.

(a) Huku ukitoa mifano **minne**, eleza hali ya kinyume inayojitokeza katika aya ya pili. (alama 4)

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(b) Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu. (alama 3)

................................................................................................................................

................................................................................................................................

................................................................................................................................

................................................................................................................................

(c) Kwa kurejelea aya ya nne, onyesha mchango wa serikali katika kuwajibikia haki za watoto. (alama 3)

................................................................................................................................

................................................................................................................................

................................................................................................................................

................................................................................................................................

(d) " Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu. (alama 2)

................................................................................................................................

................................................................................................................................

................................................................................................................................

(e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)

(i) vigogo................................................................................................

(ii) huwa nanga kwao................................................................................

(iii) kujikuna wajipatapo...........................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

2 **UFUPISHO**: (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Wataalamu mbalimbali wamekuwa wakifanya utafiti kuhusu Ziwa Viktoria. Juhudi hizi za uchunguzi zimekuwa zikionyesha kwamba ziwa hili ambalo ndilo la pili kwa ukubwa miongoni mwa maziwa yenye maji matamu duniani linaangamia taratibu. Inakisiwa kuwa kukauka kwa ziwa hili kutahatarisha maisha ya watu zaidi ya milioni 30 ambao hulitegemea kwa chakula na mapato. Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Masuala ya Bahari na Uvuvi nchini ulionyesha kuwa Ziwa Viktoria linaangamia kwa kiasi cha mita tatu kila mwaka. Hivi sasa baadhi ya fuo zilizokuwa kwenye ziwa hili upande wa Kenya zimekauka. Mandhari ya fuo hizi nayo yameanza kutwaa sura mpya. Badala ya kupata madau na wavuvi wakiendesha shughuli zao katika maeneo haya, huenda isiwe ajabu kupata watoto wakicheza kandanda.

Rasilimali za samaki ziwani humu zinaendelea kudidimia huku wavuvi wakitupwa kwenye biwi la umaskini. Walisema wasemao kwamba akosaye la mama hata la mbwa huamwa. Wavuvi wamebuni mikakati ya kukabiliana na hali hii ambayo inatishia kukiangamiza kizazi chao. Wengi wao wameamua kufanya biashara maarufu kwa jina, 'bodaboda,' wengine wameingilia kilimo baada ya kushindwa kujikimu kimaisha kutokana na uvuvi. Wavuvi wanaoendelea kuvua samaki katika ziwa hili wamejipata katika hali ngumu ya kiuchumi. Hali hii imewalazimisha baadhi yao kuanza kuvua samaki katika maji ya mataifa jirani; jambo ambalo limewachongea, wengi wakatiwa mbaroni huku wengine wakinyanyaswa na maafisa wa usalama wa mataifa hayo jirani.

Sekta ya uchukuzi na mawasiliano nayo imeathirika si haba. Shughuli za uchukuzi katika ziwa hili zimetingwa na gugu-maji ambalo limetapakaa kote ziwani. Mbali na gugu-maji hili, shughuli za kilimo cha kunyunyizia maji zimetanzwa. Kadhalika, kupungua kwa viwango vya maji humu ziwani ni changamoto nyingine ambayo inawashughulisha wanaharakati wa mazingira. Inahofiwa kuwa mataifa ya Afrika Mashariki yanalipoteza ziwa hili hatua kwa hatua. Hakika, wanasayansi wa masuala ya bahari wameonya kuwa ziwa hili litakauka katika kipindi cha karne moja ijayo!

Ni dhahiri kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ina jukumu la kulitunza ziwa hili kwa jino na ukucha. Serikali za nchi husika, hususan Kenya, Uganda na Tanzania zinapaswa kutekeleza sheria zinazodhibiti shughuli za uvuvi katika ziwa hili. Mathalan, kuna haja ya kuvua kwa misimu ili kukinga dhidi ya kuangamia kwa rasilimali za samaki. Wavuvi nao hawana budi kushauriwa

kuhusu umuhimu wa kufuata kanuni za uvuvi zilizowekwa na kutahadharishwa kuhusu madhara ya kuendesha uvuvi kiholela. Sheria kuhusu aina za nyavu za kuvulia pia inapaswa kutekelezwa vilivyo. Aidha, kuna haja ya serikali za muungano huu kukomesha shughuli za kilimo kandokando mwa ziwa hili, pamoja na kwenye mito iliyo katika ujirani wa ziwa lenyewe. Hatua hii itasaidia kukomesha kusombwa kwa udongo na mbolea kutoka mashambani hadi ziwani. Hali kadhalika, muungano huu unapaswa kuweka sheria za kusimamia matumizi ya maji. Hili litawadhibiti raia wenye mazoea ya kubadhiri maji.

Isitoshe, serikali za mataifa ya Afrika Mashariki hazina budi kuchunguza viwanda vinavyotupa taka ndani ya ziwa hili. Mbali na kuchafua maji, viwanda hivi vinaangamiza mimea na wanyama wa majini. Uchunguzi huo unapaswa pia kuhusisha mito inayomimina maji katika ziwa hili. Viwanda vyote vinavyotumia maji ya mito kama vile: Nzoia, Yala, Sondu-Miriu, Awach, Kuja na Kagera vinastahili kuchunguzwa pia.

Juhudi za kufikia ustawi wa kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki zinapaswa kutilia maanani uhifadhi wa Ziwa Viktoria. Kukauka kwa ziwa hili ni sawa na kukauka kwa maazimio na ndoto zote za serikali za nchi husika za kuboresha hali ya maisha ya raia wake. Wakati ni sasa.

(a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 70 - 75. (alama 9, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Nakala safi:**

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

(b) Huku ukitumia maneno 50 - 55, eleza masuala muhimu ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama 6, 1 ya mtiririko)

**Matayarisho:**

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Nakala safi:**

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

3 **MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

(a) Huku ukitoa mfano, fafanua dhana ya mzizi wa neno. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(b) Onyesha matumizi ya kiambishi **'ku'** katika sentensi ifuatayo:

Amani atakutengenezea mpini wa jembe kisha aelekee kule kwao. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(c) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) Irabu ya mbele, wastani ....................................................................................

(ii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini ....................................................................

(d) Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya YA - YA kutunga sentensi. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(e) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali timilifu. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(f) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)

KN (N) + KT (T + E) + U + KN (N) + KT (T + E)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(g) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi changamano. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(h) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya: **koga** na **konga**. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(i) Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na nomino ya jamii. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(j) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (alama 3)

(i) nywa (tendesha) ..........................................................................................

(ii) la (tendeana)..............................................................................................

(iii) vaa (tendwa) ..............................................................................................

(k) Akifisha sentensi ifuatayo kubainisha dhana **tatu** tofauti.

Julius Kiptoo mwanawe Kung'u na Justine walikiletea kijiji chao sifa. (alama 3)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(l) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari.

Naam, ameleta machache. (alama 2)

..........................................................................................................................

(m) Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu. (alama 2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(n) (i) Eleza maana ya shadda. (alama 1)

..........................................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

(ii) Onyesha panapotokea shadda katika neno: ' mteremko'. (alama 1)

..............................................................................................................

(o) Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

Sahibu yake alishikwa na kisunzi.

..............................................................................................................

(p) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari.

Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na viongozi wenye misimamo thabiti mno.

(alama 3)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(q) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.

" Shughuli yetu itamalizika kesho, " mama alimwambia Juma. (alama 2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(r) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo:

Watahiniwa hao walisoma maswali yote kwa makini. (alama 2)

..............................................................................................................

(s) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu/dhamira yake.

Funga majani matano matano kwa kila fungu. (alama 1)

..............................................................................................................

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

4 **ISIMUJAMII** (Alama 10)

Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha.

(a) Mazingira (alama 4)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(b) Madhumuni (alama 2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(c) Malezi (alama 4)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

**<u>KISWAHILI KARATASI YA TATU</u>**